

Wakaguzi wapewa angalizo ukaguzi mifumo TEHAMA

Na Romana Mallya

MKURUGENZI Mkuu wa Ndani Msaidizi Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali, Paison Mwamnyasi, amewataka wakaguzi wa ndani kuzingatia sheria, kanuni, viwango na miongozo ya serikali mtandao wanapofanya ukaguzi katika miradi na mifumo ya TEHAMA ili kutoa ushauri wenye tija serikalini kupitia taarifa zao za ukaguzi.

Alielekeza hayo wakati wa ufunguzi wa awamu ya pili ya mafunzo maalum kwa wakaguzi wa ndani kutoka Mamlaka 13 za Serikali za Mitaa yaliyofanyika mkoani Morogoro juzi.

Alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa

wakaguzi wa ndani kwa kuwa yanawajenga uwezo katika utendaji kazi na kurahisisha shughuli za ukaguzi na kutoa ushauri wenye tija kwa serikali.

"Ukielewa namna mifumo inavyofanya kazi, unaweza kukagua ipasavyo na tutaeputa kutaja majina ya watu katika taarifa zetu za ukaguzi badala ya mifumo.

"Sisi wakaguzi tunatambua kuwa miongozo ya ukaguzi inaeleza kutokagua sehemu ambayo hauna uelewa nayo kwa kuwa unaweza kutoa maoni na ushauri kwa serikali ambao hauna tija," alisema.

Mkurugenzi wa Udhibiti na Usalama wa TEHAMA Mamiaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Sylvani Shayo, aliwasisitiza wakaguzi wa ndani kutumia sheria, kanuni, viwango

na miongozo ya serikali mtandao wakati wa kusimamia na kufanya ukaguzi wa miradi na mifumo ya TEHAMA katika taasisi zao.

Alisema e-GA kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wanaendelea na jitihada za kutoa mafunzo kwa kundi hilo ili kufanya ukaguzi kwa ufanisi.

"Ikiwa wakaguzi wa ndani mtazingatia vyema miongozo na sheria hizo mtafanya ukaguzi wenye tija na masiahi kwa taifa," alisema.

Meneja wa Udhibiti wa Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao, Sultana Seiff, alisema e-GA haitaki kuacha kada yoyote nyuma katika matumizi ya TEHAMA kwa kuwa dunia ya sasa inaendeshwa

kidijitali.

Alisema wakaguzi wa ndani wanapewa mafunzo hayo ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na kuboresha utoaji wa huduma za serikali kwa njia ya kidijitali.

Mafunzo hayo ya siku tano yanayofanyika mkoani Morogoro yalianza Juni 5, mwaka huu, yakihusisha wakaguzi wa ndani 110 kutoka halmashauri na za mikoa ya Dodoma, Tabora, Singida, Kigoma, Mara, Dar es Salaam, Morogoro, Shinyanga, Rukwa, Kagera, Geita, Simiyu na Katavi.

Awamu ya kwanza ya mafunzo hayo ilikuwa mwezi Machi mwaka huu, wakaguzi wa ndani 133 kutoka halmashauri za mikoa 13 za Tanzania Bara walishiriki